


Jinsi Viumbe wa Roho Wanavyohusika Maishani Mwetu (Sehemu ya 1)

Inategemea sura ya 10 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza yale unayoamini na sababu inayokufanya uamini hivyo, chunguza yale ambayo Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine yale unayoamini.



MALAIKA NI NANI?

1 CHUNGUZA YALE UNAYOAMINI

Watu wengine wanaweza kusema nini?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA YALE AMBAYO BIBLIA INAFUNDISHA

Malaika ni viumbe wa roho wenye nguvu, akili na hisia.

(Ona sura ya 10 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 1-5.)

Soma Ayubu 38:4-7, Zaburi 103:20, na Luka 15:10.

Mistari hiyo inaonyeshaje kwamba malaika wana nguvu, akili, na hisia?

Soma Danieli 6:22 na Matendo 12:6-11.

Malaika waaminifu waliwasaidiaje watumishi wa zamani wa Mungu?



Malaika hushangilia hata mtu mmoja anapomrudia Yehova.—Luka 15:10

Si malaika wote walio waaminifu.

(Ona sura ya 10 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 6-8.)

Soma Ufunuo 12:9.

Kulingana na mstari huo, je, ni Shetani Ibilisi pekee ndiye aliyeasi?

Soma Mwanzo 6:2.

Roho waovu walimwasi Mungu jinsi gani?

Soma Zaburi 34:7.

Unahisije kujua kwamba Mungu huwatumia malaika waaminifu kutulinda kutokana na malaika wanaotaka kutudhuru kiroho?

3

ELEZA YALE UNAYOAMINI

IKIWA MTU ANASEMA...

Malaika hawapo.

UNAWEZA KUMWAMBIA...

Watu wengi wana maoni kama hayo. Lakini mimi siamini hivyo kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?

IKIWA MTU ANASEMA...

Sijawahi kuwaona malaika, hivyo hawawezi kunisaidia maishani.

UNAWEZA KUMWAMBIA...

Ni kweli kwamba malaika hawawatokei wanadamu kama walivyofanya katika nyakati za Biblia. Lakini ninaamini kwamba *wanahusika* katika maisha yetu kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?
